


TOLEO MAALUM LA MKOA WA
DAR ES SALAAM





# TEMEKE YANGARA KWA MAENDELEO YA WANANCHI WAKE



Mhe. Felix Lyaniva
Mkuu wa Wilaya Temeke

Na Joyce Msumba- Afisa Uhusiano

Temeke inajulikana nchini, kutokana na umaarufu wake, ni ukweli usiopingika, kuanzia historia yake, miundombinu yake, uwepo wa viwanja vikubwa nchini vya michezo, bandari, mandhari ya kuvutia ikipambwa na daraja la Kigamboni, busara za viongozi wake kutokana na usimamizi wa maendeleo ya wananchi wake, na hasa katika kugawana mali na Manispaa ya Kigamboni bila vurugu hata kufikia kupongezwa na uongozi wa Mkoa wa Dar-es-Salaam.

Haya yalidhihirishwa tena na Bibi Theresia Mbando, Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar-es-Salaam alipohudhuria kikao cha baraza la Madiwani hivi karibuni katika ukumbi wa kumbukumbu ya Idd Nyundo Marehemu, aliyekuwa Mkurugenzi 1999 hadi 2008.

Kikao hicho kilikuwa maalum cha kupitia hoja za ukaguzi wa hesabu za serikali zilizowasilishwa na Mkaguzi Mkuu wa nje wa Wilaya ya Temeke Bibi Alestidia Ngalaba.

Bibi Mbando alimuwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Dar-es-Salaam Mhe. Paulo Makonda kama mgeni rasmi katika kikao hicho, aliipongeza Wilaya pamoja na Halmashauri ya Manispaa ya Temeke yenye kuongozwa na Mhe. Felix Lyaniva Mkuu wa Wilaya hii, Mstahiki Meya Abdallah Chaurembo, Bwana Nassib Mbagga Mkurugenzi, baraza la Madiwani pamoja na watendaji wote kwa ujumla kwa kuiletea sifa Temeke kwa kupata HATI SAFI mfululizo kwa miaka minne, kuanzia 2012/2013 hadi 2015/2016.

Vile vile kwa kuwa wa kwanza Kimkoa katika maonesho ya nanenane yaliyopita kikanda mjini Morogoro, na siri kubwa ya ushindi huo ni uthubutu wa kuwa na wazalishaji wa bidhaa ndogo ndogo za kusindikwa na viwanda unaofanywa na wajasiliamali waliowezeshwa mitaji itokanayo na Mkurugenzi kupitia DCB, SACCOS, na wanufaika na mfuko wa jamii wa TASAf.Vile vile kwa vipando vya aina mbali mbali vilivyolimwa na wakulima wenyewe, na kwa kuwa na klinik ya mimea na matumizi ya madawa asili kuzuia na kuua wadudu wa mimea.

Bidhaa hizo za wajasiliamali katika banda zilikuwa ni kivutio kikubwa katika maonesho haya na fundisho kwa wale waliotembelea . "Jukumu letu sasa ni kuwatafutia masoko, na nawaomba City FM radio, redio ya Jiji la Dar-es-Salaam, katika vipindi vyenu mjulishe umma juu ya upatikanaji wa bidhaa hizi, hayo yalisemwa na Mhe. Abdallah Chaurembo Meya wa Halmasahuri ya Temeke akizungumza na mwandishi wa Radio ya Jiji hili.

Kwa upande mwingine Mstahiki Meya wa Manispaa ya Temeke,Mhe. Abdallah Chaurembo, aliiongezea sifa halmashauri yake mbele ya mgeni rasmi alisema,Halmashauri ya Manispaa ya Temeke ni sikivu kwa maagizo yatolewayo na serikali kuu.

Sifa nyingine ya Halmashauri ya manispaa ya Temeke ni kuwa ya kwanza kimkoa katika utekelezaji wa Mradi wa DMDP {Dar-es-salaam Metropolitan Development Project} unaofadhiliwa na Benki ya Dunia, nguvu hizo zilitokana na uongozi, baraza na menejimenti kwa kutoa maamuzi kwa wakati, kama vile,jinsi ilivyoitikia wito wa kutafuta fedha za kulipa fidia wananchi wake wanaopisha mradi katika maeneo yao ya makazi na mali nyingine, vile vile kutenga fedha za ujenzi wa vyumba vya madarasa, maabara na ununuzi wa madawati kwa shule za msimgi na Sekondari.




# MAFANIKIO NDANI YA MANISPAA YA TEMEKE KWA MWAKA 2016/2017



Bw. Nassib Mmbagga Mkurugenzi Manispaa ya Temeke

Mheshimiwa Waziri Mkuu Majaliwa Kassim Majaliwa katika kikao chake Kikuu cha ALAT akiwa na waheshimiwa Mameya, aliwaagiza kuwa; endapo kutakuwa na halmashauri itakayoshindwa kufikisha zaidi asilimia 80 ya mapato yake ya ndani basi itafutwa.

Halmashauri ya manispaa ya Temeke, katika mwaka wa fedha 2016/2017 ilipanga kukusanya kiasi cha shilingi za kitanzania 181,528.681,515 kutokana na ruzuku ya serikali kuu, vyanzo vya ndani, wahisani na nguvu za wananchi, katika kiasi hicho shilingi bilioni 31.8 zingetokana na vyanzo vyake vya ndani,hata hivyo ilifanikiwa kukusanya bilioni 26 hivyo kuweza kutimiza agizo la Waziri Mkuu kwa asilimia 83.

Pamoja na mafanikio hayo, bado kulikuwa na changamoto zilizojitokeza ndani ya mwaka huo wa fedha, kwani baadhi ya vyanzo vikuu vya mapato ya ndani vilichukuliwa serikali kuu, ikiwemo kodi ya majengo. Kodi ya majengo ilikuwa ni tegemeo kubwa kwa makadirio ya kukusanya shilingi bilioni 10, Halmasahuri ilipokea milioni 390 kama rejesho la mapato.

Changamoto nyingine ni upungufu wa idadi ya watumishi, kabla na baada ya zoezi la kuhakiki vyeti, idadi kamili ya watumishi waliopo hivi sasa ni 6,628 na pungufu ni watumishi 1,451.



Baraza la madiwani.



Daraja la Nyerere

Hata hivyo halmashauri ya Manispaa ya Temeke ilitumia kiasi kilichokusanywa katika kuboresha miradi ya maendeleo na kutoa huduma kwa wananchi wake, katika kukamilisha miradi viporo na kujenga miundombinu mingine mipya ya barabara za lami na za changarawe, Ujenzi na ukarabati wa zahanati na hospitali ya Rufaa ya Temeke, Ujenzi wa madarasa na uchimbaji wa visima virefu vya maji.

Ujenzi wa barabara za lami na changarawe, ulitengewa kiasi cha shillingi bilioni 8.3, na kufanikiwa kutumia kiasi cha shilingi bilioni 5.2 sawa na asilimia 63 ya fedha zilizotokana na vyanzo vyetu vya ndani pamoja na michango kutoka serikali kuu na Wahisani.

Kutokana na fedha za mfuko wa barabara, jumla ya shilingi bilioni 7.9 zilitumiwa katika ujenzi wa barabara ya Saku Kata ya Chamazi, barabara ya kwa-Pazi Kata ya Charambe, barabara ya Kwa-Ndunguru Kata ya Kibondemaji pamoja na kufanya marekebisho madogo madogo katika barabara nyingine ndani ya Mitaa.

Sekta ya Afya, halmashauri ilipanga kutumia kiasi cha shilingi bilioni 3.9 kutoka serikali Kuu, na kupokea bilioni 2.7 sawa na asilimia 70 ya makadirio, wahisani milioni 374, lakini ilipokea shilingi milioni 42 sawa na asilimia 11.

Hata hivyo fedha hiyo ilitumika kukamilisha ujenzi wa zahanati kubwa na ya kisasa ya Charambe,muendelezo wa ujenzi wa kituo cha Afya Kijichi , ukarabati wa zahanati ya wazazi Round table, maboresho madogo madogo hospitali ya Zakhem, na hospitali ya Temeke.

Sekta ya Elimu, katika mwaka wa fedha 2016/17, halmashauri ya manispaa ya Temeke ilipata changamoto kwa kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi katika shule zake za msingi kuliko uwezo wake, shule hizo ni Maji matitu (6,456 sawa sawa na shule 6), Msufini ( 4,112 sawa na shule 3 ), Chamazi (4,537 sawa na shule 3 ), na Mbande( 6,274 sawa sawa na shule 6).

Halmashauri ilipokea fedha kutoka Ofisi ya Rais, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Wizara ya elimu, sayansi na Teknolojia (P4R)pamoja na mapato yetu ya ndani kwa ujenzi wa vyumba 117 na kununulia madawati 1,3948.

Mhe. Seleman Jaffo, Naibu Waziri TAMISEMI, alipotembelea shule hizo wakati wa ziara yake Temeke, Bibi Silvia Mutasingwa Kaimu Afisa Elimu Msingi alimwambia Waziri kuwa ; pamoja na kwamba wanafunzi wote wanakalia madawati, lakini bado inakuwa vigumu katika suala la usimamizi wa watoto hao hasa kwa shule za Mbande, Maji matitu, Chamazi na Misufini, naye Waziri alishauri shule hizo zigawanywe kuwa mbili mbili kila moja wakati utaratibu mwingine ukifuata.

Elimu ya Sekondari vilijengwa vyumba vya madarasa 564, ofisi za walimu 7, na ununuzi wa madawati 2,560 .



Zahanati ya Charambe

TOLEO MAALUM LA MKOA WA
DAR ES SALAAM

# MRADI WA DMDP MANISPAA YA TEMEKE

Halmashauri ya manispaa ya Temeke ina jumla ya Kata 23, kati ya Kata hizo 16 zimeingia katika mradi wa DMDP (Dar-es-Salaam Metropolitan Development Project) unaofadhiliwa na Benki ya Dunia kiasi cha dolla za kimerikani bilioni 600 kwa Mkoa wa Dar-es-Salaam, kutokana na fungu hili, Temeke imepokea shilingi bilioni 222, fedha ambayo itatumika katika ujenzi wa nyumba za bei nafuu kwa wananchi na kupima viwanja vya makazi 800 maeneo ya Vikunai Kata ya Toangoma.

Vile vile mradi utajenga barabara za lami zenye urefu wa kilometa 90, kabla ya ujenzi huo, manispaa ya Temeke ilikuwa na mtandao wa barabara zenye urefu wa kilometa 70 zikiwa ni za barabara za lami, hivyo Temeke kwa msaada huo itakuwa na kilometa za barabara za lami 160.

Barabara hizo za lami zitakuwa na taa za mitaani, miradi mingine ni mifereji mikubwa ya maji ya mvua, masoko 4 ya kisasa, Vituo 4 vya mabasi, zahanati ya Makangarawe na kiwanja cha mpira, pamoja na makontena ya ukusanyaji taka na ujenzi wa kituo cha Afya,.

Hayo yalisemwa na Bwana Edward Simon, Mratibu wa Mradi wa DMDP manispaa ya Temeke, alipohojiwa na mwandishi wa habari hii, akiendelea alisema mpaka hivi sasa wakandarasi wanaendelea na kazi katika maeneo ya mradi.

Bwana Edward alisema kiasi cha shilingi bilioni 21.6 zinatumika katika ujenzi wa barabara ya Mwanamtoti yenye urefu wa kilometa 1.8, inayojengwa kwa kiwango cha lami, barabara hiyo inayonganisha barabara ya Kilwa na barabara ya Kijichi Toangoma yenye urefu wa kilometa 3,ndani yake kukiwa na daraja lenye urefu wa mita 16 pamoja na ujenzi wa jengo la ofisi la mradi pamoja na maabara ghorofa moja .

CRJE Kampuni ya ujenzi kutoka nchini china ndiyo inayojenga daraja na barabara ya Kijichi Toangoma, jengo la ofisi la mradi pamoja na maabara ya kisasa ambayo itatumika kupima udongo wa barabara zote zitakazojengwa , Kampuni hii ilijenga daraja la Kigamboni.

Ujenzi wa mradi wa barabara na madaraja kijichi Toangoma ulisainiwa tarehe 15 mwezi Februari mwaka huu, na unategemewa kukabidhiwa mwezi Februari 14 mwaka 2018, wakati ujenzi wa ofisi unategemewa kukamilika na kukabidhiwa mwezi Septemba mwaka huu.



DMDP OFISI

Mpaka hivi sasa ujenzi wa barabara ya Mwanamtoti umefikia asilimia 36, na ule wa barabara ya Kijichi Toangoma imefikia asilimia 40. Kukamilika kwa ujenzi wa barabara hizi, kutafungua mtandao wa barabara kutoka maeneo ya Kigamboni kuelekea Ubungo kwa kutumia barabara ya Kilwa, na ama kwenda Uwanja wa ndege kwa kupitia Nzasa Kilungule Barabara ya Buza.

Wajibu wa kulipa fidia wakazi ili wapishe mradi lilikuwa ni jukumu la serikali, hata hivyo halmasahauri ya Manispaa ya Temeke kupitia maamuzi ya baraza na mejimenti ilifanikiwa kwa asilimia kubwa kuwalipa wakazi wa Kata husika ili kupisha mradi uanze mapema, kiasi cha bilioni 18zimeshalipwa kati ya bilioni 20.3 zilizokusanywa, na wakazi 2,100 wa maeneo mbalimbali zimetumika wameshalipwa na zoezi hilo linaendelea Kata ya Kilakala hivi sasa.



Banda la Nane nane Mjini Morogoro

**Vile vile mradi utajenga barabara za lami zenye urefu wa kilometa 90, kabla ya ujenzi huo, manispaa ya Temeke ilikuwa na mtandao wa barabara zenye urefu wa kilometa 70 zikiwa ni za barabara za lami, hivyo Temeke kwa msaada huo itakuwa na kilometa za barabara za lami 160.**




# MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA UJAO





Ujenzi wa barabara na dara la Kijichi Toangoma

Halmashauri ya manispaa ya Temeke, ina mpango mzuri wa kuwaletea wananchi wake maendeleo, kutatua kero zao na kuboresha utoaji wa huduma kutokana na makusanyo ya mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani,Ruzuku kutoka serikali kuu na wahisani.

Kutokana na kubuni vyanzo vipya vya mapato ambavyo havitamnyanyasa mwananchi.Vile vile kuendelea kutoa elimu kwa wananchi wake juu ya ulipaji kodi kwa hiari.

Akizungumzia kuhusu ukusanyaji wa mapato ya ndani katika Baraza la madiwani, Mstahiki Meya Chaurembo aliwaambia wajumbe wa baraza kuwa waheshimiwa madiwani walienda kujifunza Mjini Tanga juu ya vyanzo vipya vya mapato ya ndani kwa kutumia bandari na kumbi za starehe, vingine ni vituo vya daladala, kuwatambua, kuwasajili na kuwapatia wamachinga maeneo ya kufanyika biashara zao ili kukusanya mapato ya ndani katika vyanzo hivi vipya na vingine vidogo vidogo na rafiki.

Aidha Mstahiki Meya akiongea katika viwanja vya nanenane Mjini Morogoro alisema ni muda sasa Halmashauri ziendelea kuwajali wajasiliamali kwa kuwapatia mitaji ya biashara zao ndogo ndogo, kuendeleza ubunifu wao wa viwanda vidogo vidogo kupitia mitaji itokanayo na Mkurugenzi wa Halmashauri na kwamba; namnukuu “Hakuna serikali duniani isiyokusanya kodi”. Kwa hili Temeke tutatoka hapa tulipo sasa na kwenda hatua nyingine ya juu zaidi alisema.



Ujenzi wa madarasa shule ya Msingi Misufini




# TAARIFA YA HUDUMA ZA AFYA, USTAWI WA JAMII NA MSAMAHA KATIKA UZINDUZI WA VITAMBULISHO VYA MSAMAHA KWA WAZEE MANISPAA YA UBUNGO

**TAREHE:04 SEPTEMBA, 2017.**



**Mhe. Ummy Mwalimu** Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto **(MB),**
Mh. Mkuu wa Wilaya ya Ubungo,
Katibu Tawala Wilaya,
Mh. Katibu wa CCM Wilaya ya Ubungo,
Mh. Mstahiki Meya wa Manispaa ya Ubungo,
Ndugu Mkurugenzi Manispaa ya Ubungo,
Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam,
Waheshimiwa Madiwani wa Manispaa ya Ubungo,
Wataalamu mbalimbali mliopo ngazi ya Mkoa na Wilaya,
Watendaji wa Kata Manispaa ya Ubungo,
Wenyeviti wa Mitaa Manispaa ya Ubungo,
Mabibi na Mabwana.
***Asalaam Aleykum, Bwana asifiwe, Tumsifu Yesu kristo.***

**Mheshimiwa Waziri.**
Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema, na kuniwezesha kusimama mbele yenu na kuwasilisha taarifa hii katika uzinduzi huu wa utoaji wa vitambulisho vya msamaha wa huduma za afya kwa wazee katika Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo.

**Mheshimiwa Waziri.**
Manispaa ya Ubungo ni Manispaa mpya iliyoanza rasmi Septemba, 2016 ikiwa ni moja kati ya Manispaa tano za Mkoa wa Dar es Salaam. Manispaa ina jumla ya vituo **19** vya umma vinavyo toa huduma mbalimbali za Afya ikiwemo huduma za msamaha kwa makundi maalum. Ambapo Hospitali ni **1**, Vituo vya Afya **3**, Zahanati **15** na Kliniki ya Mama na mtoto **1.**
Hadi kufikia tarehe **22/08/2017** Manispaa imeweza kuwatambuwa jumla ya wazee **7,299** kutoka Kata **11** na Kata **3** zilizobaki utambuzi unaendelea.

Kati ya wazee **7,299**, (**Me** ni **3,454** na **Ke 3,845**). Jumla ya wazee **2,051** (**Me 1,214** na **Ke 837**) tayari wameshapigwa picha na kazi ya kudurufu vitambulisho vyao inaendelea. Wazee **5,248** waliobaki kazi ya upigaji picha inaendelea katika Kata husika.

**Mheshimiwa Waziri.**
Wazee hawa wametambulika kupitia Kata zao husika kwa vigezo vifuatavyo:-
- Wazee wasiojiweza kuanzia umri wa miaka **60** na kuendelea.
- Awe mkazi wa Manispaa ya Ubungo, Mkoa wa Dar es salaam.
- Awe amejiandikisha kupitia Mtendaji Kata husika.
- Awe amepigwa picha.

Aidha Manispaa ya Ubungo imelenga kukamilisha zoezi la utambuzi na utoaji wa vitambulisho vya msamaha wa huduma za Afya kwa wazee wote **7,299** ifikapo Septemba, 30 mwaka 2017.

**Mheshimiwa Waziri.**
Nichukue fursa hii pia kwa niaba ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Ubungo, kuishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamiii, Jinsia, Wazee na Watoto ambayo ndio imebeba dhamana kubwa ya kuhakikisha Afya za wananchi zinaboreshwa kwa kupata huduma bora za tiba na kinga kwa makundi yote ya kijamii.
Uzinduzi huu wa vitambulisho vya wazee tunaoufanya leo ni moja ya utekelezaji wa ***Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2015 – 2020 sura ya nne, ibara ya 50 (P)*** *,ambayo inasema "…****Aidha HALMASHAURI zitahakikisha WAZEE wanatambuliwa na kupewa***








***MATIBABU BURE katika Hospitali za Serikali”*** Hivyo Manispaa ya Ubungo imetekeleza ahadi hii kwa vitendo Lakini pia ni jitihada na hatua mahsusi zinazochukuliwa na Serikali ya awamu ya tano chini ya Rais wetu mpendwa, **Dr. John Pombe Joseph Magufuli,** kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kuhakikisha Wazee wakitanzania wanakuwa na afya bora.

**Mheshimiwa Waziri.**

Pamoja na utekelezaji huu Manispaa ya Ubungo tumekuwa tukikutana na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa huduma za afya kwa ujumla wake, Changamoto hizo zikiwa ni:-

- Gharama za uendeshaji wa huduma za msamaha zimekuwa ni kubwa hususani katika Hospitali yetu ya Wilaya Sinza, ambapo kwa Mwaka wa fedha **2016/2017** ilikuwa ni ***shilingi bilioni moja, million mia nane na tano, laki tisa thelathini na nne elfu na mia mbili* (1,805,934,200/=),** ambapo ni zaidi ya ukomo wa bajeti ya Hospitali ya bilioni moja na milioni kumina tano **(1,015,000,000)** kwa vyanzo vyote vya mapato vya Hospital. Hii ni kutoka na idadi kubwa ya wagonjwa wanaohitaji msamaha, wakiwemo akina mama wajawazito, watoto chini ya miaka mitano na wazee.
- Hospitali ya Wilaya tuliyonayo imekuwa na changamoto ya ufinyu wa nafasi ya wodi za kulaza wagonjwa pamoja na kutokuwa na chumba cha kuhifadha maiti **(Mortuary).**
- Upungufu wa watumishi katika Kada mbalimbali za Afya unaojumuisha Madaktari, Wauguzi na wataalamu wa Maabara.
- Upungufu wa Magari ya kubeba wagonjwa **(Ambulance).**
- Upungufu wa gari kwa ajili ya huduma za chanjo na usimamizi shirikishi.

**Mheshimiwa Waziri.**

Pamoja na changamoto hizo zinazoikabili Halmashauri yetu ya Ubungo kwa Idara ya Afya na Ustawi wa Jamii, tumekuwa na mikakati mbalimbali ya kutatua changamoto hizo:-

- Kwa mwaka huu wa fedha 2017/2018 zaidi ya 33.3% ya ukomo wa bajeti tuliyopewa imetengwa kwa ajili ya kununua dawa na vifaa tiba. Aidha tunaomba kuongezewa mgao wa ruzuku ya dawa kutoka Serikali kuu kwa Hospitali ya Sinza ilikuweza kukabiliana na uwingi wa wagonjwa tunao wahudumia.
- Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 tumetenga kiasi cha fedha Tsh. 200,000,000/= kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa ghorofa 4 Sinza Hospitali na ujenzi huo utafanyika kwa awamu kulingana uwepo wa fedha.
- Kwa upande wa chumba cha kuhifadhi maiti itazingatiwa kwa mwaka wa fedha ujao 2018/2019.
- Idara ya Afya na Ustawi wa Jamii ina jumla ya watumishi 564. Ambao bado hawatoshelezi. Hivyo tuna upungufu wa watumishi 268 ilikufikia Ikama ya 832.
- Kwa sasa Halmashauri ya Ubungo ina magari mawili ya kubeba wagonjwa (Ambulance).Hivyo Mhe. Waziri kupitia ofisi yako tunaomba utufikirie kwenye mgao, kwa kuanzia tunaomba tupate magari mawili ili kuboresha zaidi huduma za dharura na rufaa.
- Sambamba na hilo Mhe. Waziri Idara ya Afya na Ustawi wa Jamii ina magari mawili kwa ajili ya huduma za kiofisi, tunaomba kufikiriwa kwenye mgao wa magari ya huduma za chanjo ili tuweze kuongeza ufanisi wa utoaji huduma za Afya Kinga kwenye Halmashauri yetu.

**Mheshimiwa Waziri.**

Baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Ubungo naomba leo hii uzindue utoaji wa vitambulisho vya msamaha kwa wazee **150**, waliopo kwenye hadhara hii ambao ni wawakilishi wa wazee **7,299** watakaopewa vitambulisho.

**Mheshimiwa Waziri.**

*Kwa niaba ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Ubungo naomba kuwasilisha.*

***Ahsante.***






# HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO

## TAARIFA YA MIRADI INAYOENDELEA KUTEKELEZWA KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA MANISPAA YA UBUNGO KWA KIPINDI CHA JULAY 2016 – JUNI 2017.

**TANGULIZI**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha **2016/2017** Halimashauri ya Manispaa ya Ubungo imeendelea na uboreshaji wa miuundombinu ya shule zote **27** za sekondari za Manispaa sambamba na ujenzi wa shule Mpya katika Kata ya **Kimara** . Miradi ya uboreshaji wa miundo mbinu hiyo inahusisha: **ukarabati** wa vyumba vya madarasa **25,** ujenzi wa vyumba vipya vya **madarsa 17,** ujenzi wa matundu ya **vyoo 40,** umaliziaji wa **maabara 3** na ujenzi wa **nyumba za walimu 7** ( Shule ya sekondari matosa **(6)** na Goba **(1)** . Baadhi ya miradi hiyo imekamilika na mingine utekelezaji wake upo katika hatua mblimbali kama ifuatavyo:

1. **UJENZI WA VYUMBA 2 VYA MADARASA, MNARA WA MAJI NA MATUNDU 8 YA VYOO VYA WANAFUNZI SHULE YA SEKONDARI MATOSA**





Mradi huu umekamilishwa kwa awamu mbili (Phase i & Phase ii), awamu ya kwanza ya utekeleza wake ulihusisha fedha za ruzuku kutoka serikali kuu ( **SEDEP**) kiasi cha **sh 85,882,760** katika awamu hii ujenzi wa madarasa **2**, jengo la choo cha wanafunzi matundu **8**, kuchimba kisima na kujenga mnara wa maji vilifanyika hadi kufikia hatua ya plasta**.** Kufuatia kutokamilika kwa mradi, Mkurugenzi wa Manispaa ya ubungo aliagiza kumaliziwa kwa mradi huu kwa fedha za ndani kiasi cha **sh.24,500,137.04** ili

2. **UJENZI WA NYUMBA SITA KWA MOJA ( 6 MULT UNIT) SHULE YA SEKONDARI MATOSA**



Mradi huu wa ujenzi wa nyumba sita kwa moja za walimu umekamilishwa kwa awamu mbili (Phase i & Phase ii ), awamu ya kwanza ya utekeleza wake ulihusisha fedha za ruzuku kutoka serikali kuu ( **SEDEP**) kiasi cha **sh 149,964,548** katika awamu hii ujenzi wa nyumba sita kwa moja, jiko, matundu sita ya choo na bafu ulifanyika hadi kufikia hatua ya kupaua na plasta**.** Kufuatia kutokamilika kwa mradi Mkurugenzi wa Manispaa ya ubungo aliagiza kumaliziwa kwa fedha za ndani jumla ya **sh.40,681,326** ili kukabiliana na tatizo la ukosefu wa nyumba za walimu katika shule hii.

3. **UJENZI WA VYUMBA 2 VYA MADARASA NA MATUNDU 8 YA VYOO VYA WANAFUNZI SHULE YA SEKONDARI LUGURUNI**

Mradi huu umekamilishwa kwa awamu mbili (Phase i & Phase ii), awamu ya kwanza ya ulitekeleza wake ulihusishwa fedha za ruzuku kutoka serikali kuu ( **SEDEP**) kiasi cha **sh 70,063,208** katika awamu hii ujenzi wa madarasa **2**, jengo la choo cha wanafunzi matundu **8** uilifanyika hadi kufikia hatua ya plasta**.** Kufuatia kutokamilika kwa mradi, Mkurugenzi wa Manispaa ya ubungo aliagiza kumaliziwa kwa mradi huu kwa fedha za ndani kiasi cha **sh.30,000,000** ili kukabiliana na tatizo la upungufu wa madasasa na matundu ya vyoo

4. **UKARABATI WA VYUMBA 8 VYA MADARASA SHULE YA SEKONDARI Y.R. MAKAMBA**
5. **UKARABATI WA VYUMBA 4 VYA MADARASA SHULE YA SEKONDARI KIBAMBA.**
6. **UKARABATI WA VYUMBA 6 VYA MADARASA SHULE YA SEKONDARI GOBA**
7. **UKARABATI WA VYUMBA 3 VYA MADARASA SHULE YA SEKONDARI FAHARI**
8. **UKARABATI WA VYUMBA 2 VYA MADARASA SHULE YA SEKONDARI MATOSA**
9. **UKARABATI WA CHUMBA 1 CHA MADARASA SHULE YA SEKONDARI MBEZI INN**
10. **UKARABATI WA CHUMBA 1 CHA MADARASA SHULE YA SEKONDARI MPIJI MAGOHE**
11. **KUENDELEZA UJENZI WA VYUMBA 4 VYA MADARASA SHULE YA SEKONDARI MBURAHATI**
12. **KUENDELEZA UJENZI WA VYUMBA 4 VYA MADARASA, OFISI 1 YA WALIMU NA MATUNDU 10 YA VYOO SHULE YA SEKONDARI SARANGA**
13. **KUENDELEZA UJENZI WA CHUMBA 1 CHA DARASA SHULE YA SEKONDARI URAFIKI**
14. **KUENDELEZA UJENZI WA VYUMBA 4 VYA MADARASA SHULE YA SEKONDARI KILUVYA**
15. **KUKAMILISHA UJENZI WA NYUMBA 1 YA MWALIMU SHULE YA SEKONDARI GOBA.**
16. **UJENZI WA JENGO LA CHOO MATUNDU 12 SHULE YA SEKONDARI FAHARI**
17. **KUKAMILISHA UJENZI WA CHOO MATUNDU 12 YA SHULE YA SEKONDARI GOBA MPAKANI**
19. **KUKAMILISHA UJENZI WA CHOO MATUNDU 12 YA SHULE YA SEKONDARI MBURUAHATI**
20. **UJENZI WA CHOO CHA WALIMU MATUNDU 2 YA SHULE YA SEKONDARI**
21. **UJENZI WA CHOO CHA MATUNDU 12 YA SHULE YA SEKONDARI GOBA**
22. **KUKAMILISHA UJENZI WA MAABARA 3 SHULE YA SEKONDARI KIBWEGERE**
23. **KUBORESHA MIUNDOMBINU YA CHOO BAADA YA UHARIBIFU WA MVUA SHULE YA SEKONDARI KIBWEGERE**

IMETAYARISHWA NA:
**IDARA YA ELIMU SEKONDARI MANISPAA YA UBUNGO**



## TOLEO MAALUM LA MKOA WA DAR ES SALAAM



# HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO

# MWAKA MMOJA WA MANISPAA YA UBUNGO NA MAFANIKIO LIKUKI



*Uzinduzi wa magari 5 kwa ajili ya kukusanya mapato,wa kwanza kushoto Mkurugenzi wa Manispaa ya Ubungo Ndg. John L. Kayombo, katikati ni Afisa utumishi Ally J. Ally na kulia ni mweka hazina wa Manispaa Bi.Jane Machicho*

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo ni moja ya Halmshauri za Manispaa tano zilizoko katika jiji la Dar es salaam nchini Tanzania.

Ni Halmashauri ambayo imegawanywa kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni tangu kuanzishwa kwake sasa Manispaa ya Ubungo imetimiza mwaka mmoja

Mtazamo wa Halmashauri ni kuwa na jamii ambayo imewezeshwa kuendana na maendeleo ya kijamii, kiuchumi na Miundo mbinu.

Malengo ya jumla ni kutoa huduma bora kwa jamii kwa kutumia rasilimali zilizoko kwa ufanisi, na kuwajengea uwezo , utawala bora na kuheshimu utawala wa sharia ambao utaboresha maisha ya jamii, Halmashauri inajipambanua kupitia uwajibikaji na utoaji huduma kwa watu.

Vyanzo vya Mapato vya Halmashauri hutegemea sana ushuru na kodi mbalimbali , vyanzo vikubwa vya mapato ni pamoja na kodi za Mabango, ushuru wa huduma za jiji, leseni za Biashara na kwa upande wa serikali kuu ni kupitia ruzuku inayotolewa katika maeneo maalumu kama Afya ,Elimu, na Miundo mbinu.

Vyanzo vya mapato havitoshelezi kukidhi mahitaji ya Manispaa ya kutoa huduma nzuri na bora, Halmashauri ya Manispaa imeweka nguvu kutoa huduma bora kwa umma na kutafuta fursa za uwekezaji.

**MAHALI**

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo imepakana na Halmashauri ya wilaya ya Kibaha kaskazini ,Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kusini mashariki na Halmashuri ya wilaya ya Kisarawe upande wa magharibi. Halmashauri ya Manispaa ya ubungo imeunganishwa na Barabara nzuri na njia zingine za mawasiliano katika jiji la Dar es Salaam na sehemu zingine za nchi . Barabara kuu zinazounganisha Halmashauri ni Barabara ya Morogoro ,Barabara ya Mandela , na Barabara ya Sam Nujoma.

**ENEO/IDADI YA WATU**

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo ina kilometa za eneo **260.40** , kutokana na Sensa ya watu mwaka 2012 Manispaa ina jumla ya watu **.......** ambapo wanaume ni **409,149** na wanawake **436,219** lakini kwa makadilio ya idadi ya watu ya mwaka 2016 Halmashauri ya Manispaa ina jumla ya watu **1,031,349** ambapo wanaume ni **499,161** na wanawake **532,188.**

**HALI YA HEWA**

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo ina hali ya hewa ya kiikweta ambayo kiujumla hali ya hewa ni ya joto na baridi kwa mwaka mzima, msimu wa joto Zaidi ni mwezi wa kumi na mwezi wa tatu lakini mwezi wa tano na wanane ni baridi. Pia kuna misimu miwili ya mvua ambayo ni msimu mrefu na msifu mfupi , msimu mfupi ni kuanzia mwezi wa kumi na kumi na mbili , msimu mrefu ni kati ya mwezi wa tatu na wa tano.

**UTAWALA.**

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo ina Tarafa mbili (2) Kibamba na Magomeni ambapo kuna kata kumi na nne (14) na mitaa tisini na moja (91) pia Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo ina majimbo mawili ya Uchaguzi , Halmashauri kimuundo inaongozwa na baraza la madiwani (full council) ambalo lina madiwani kumi na nne (14) wa kuchaguliwa na wabunge wawili (2) wa kuchaguliwa katika Majimbo.

**MAFANIKIO.**

Manispaa ya ubungo imetimiza mwaka mmoja huku ikiwa lulu katika kusimamia na kutekeleza masuala mbalimbali kama dhamira na Malengo ya Manispaa inavyosema unaweza jionea mafanikio ya Ubungo katika mtiririko huu.

**Uboreshaji wa Usafi na Mazingira**

Katika eneo hili tunazungumzia udhibiti wa taka ngumu, udhibiti wa maji taka, uelimishaji wa jamii katika usafishaji wa Mazingira yanayowazunguka, utafiti na uendelezaji wa teknolojia kwa kutumia taka kuwa malighafi ( Composting / Recycling / Reuse ) , Upendezeshaji Manispaa (Beautification)

Hali ya uzalishaji na uzoaji taka Manispaa ya Ubungo kwa wastani huzalisha taka ngumu kiasi cha tani 828 kwa siku na Manispaa kwa imefanikiwa kudhibiti taka hizo ambapo taka zinazozolewa na kupelekwa dampo ni tani ni tani 422 sawa na 51%, Kiasi kinachorejerezwa tani 157 sawa na 19%, kiasi kinachodhibitiwa kwenye maeneo ya uzalishaji wake ni tani 142 sawa 17% , Kiasi kinachokadiliwa kubaki ni tani 108 sawa na 13%.

Kwa ujumla katika eneo la Uboreshaji mazingira Manispaa imefanikiwa kuimarisha mfumo wa ukusanyaji ada ya Taka kwa njia ya kielektroniki ambayo imesaidia ukusanyaji wa kutosha katika ngazi za kata na mitaa aidha kila mtaa umepatiwa mashine(POS machine) kwa ajili ya ukusanyaji.

Manispaa imeendelea kusimamia usafi na mazingira kiasi cha kuibuka mshindi wa kwanza ngazi ya mkoa na kitaifa kushika nafasi ya 6 katika mashindano ya kitaifa yanayoandaliwa na wizara kwa upande wa Halmashauri za Manispaa Tanzania.

**Usimamiaji wa sheria katika kushinda au kufikia suluhu kesi mbalimbali zilizokuwa mahakamani.**

Hadi kufikia septemba 26,2017 Manispaa ya ubungo imefanikiwa kumaliza jumla ya kesi kumi na sita (16) kwa kushinda na kufikia suluhu katika mahakama mbalimbali bila kuingizia Manispaa gharama.

Kutokana na Ushindi wa kesi hizo Halmashauri ya Manispaa ya ubungo imeweza kuokoa kiasi cha pesa 924,000,000

**Utekelezaji wa Huduma za Maji**

Huduma ya maji kwa wakazi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo, kwa kiasi kikubwa hutolewa na Mamlaka ya Maji ya Mjini Dar es Salaam (DAWASA) ambayo imekodisha shughuli za utoaji huduma kwa kampuni ya DAWASCO. Maji yanayozalishwa yanakidhi mahitaji kwa asilimia **65** yaani wakazi **670377** kati ya wakazi **1031349** wananufaika na huduma hiyo.

Mnamo tarehee 18/10/2016 Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Paul Makonda alituhaidi kutupatia visima kumi (10)katika Manispaa yetu ya Ubungo.

Mnamo tarehe 10/02/2017 kazi ya utafiti wa maji chini ya ardhi ulianza na kupima maeneo yote kumi(10) yaliyopo katika Manispaa yetu ya Ubungo.

Kazi ya uchimbaji ya visima hivyo kumi ilianza Mnamo mwezi wa 10/04/2017 na kukamilika mwezi wa sita.

Kwa ujumla kazi hii ya uchimbaji wa visima hivi imefanywa na wakara wa uchimbaji wa serikali (DDCA) Kwa mkataba na DAWASA wenye No AE/033/2016-2017/WC/25 Tsh **196,900,000** na ni wa siku 60.

Kazi ya Manispaa ilikua ni kusimamia pamoja na kubaini maeneo yanayoitajika na uchimbaji wa visima hivyo.

Visima hivyo vimechimbwa katika maeneo ya :-

1-Mtaa wa matosa 144M --14400L/H
2-S/Msingi Tegeta A 150M---4400L/H
3-Mtaa wa Kingazi A 162M---17400L/H
4-Mtaa wa Kingazi B 180M---18000L/H
5-Mpiji Magohe –kwa mvungi 150M---19500L/H
6-Shule ya Msingi kibesa 150M---5400L/H
7-Shule ya Msingi Makabe 150M—4400L/H
8-S/sekondari ya Gogoni 162M---18000L/H

**Sekta ya afya**

Manispaa ya Ubungo katika kipindi cha mwaka mmoja imeweka historia katika sekta ya afya kwa kutekeleza kwa vitendo maagizo ya Wizara ya Afya kwa kuwatambua wazee takribani 7299 ambao wanaumri kuanzia miaka 60 na kuendelea wazee hao wamepatiwa vitambulisho maalumu vitakavyowawezesha kupata matibabu bure.

Tayari Manispaa ya Ubungo ilishafanya uzinduzi wa vitambulisho hivyo ambao ulifanyika katika viwanja vya TP Sinza tarehe 4/09/2017 Mgeni rasmi alikuwa Waziri wa Afya Ustawi wa Jamii Jinsia Wazee na Watoto Mhe. Ummy Mwalimu.

**Ukusanyaji wa Mapato**

Katika kipindi cha mwaka mmoja Manispaa ya Ubungo imekuwa ikijihimarisha katika kuhakikisha inakusanya mapato kwa kiasi kikubwa kwa kutumia njia ya kieletroniki, moja ya jitihada ni kusogeza huduma karibu kwa kufungua kituo cha kukusanya Ada na tozo mbalimbali katika kituo cha daladala Sim 2000 sehemu ambayo wakazi na wafanya biashara katika kata za Sinza, Kimara, Ubungo ,Manzese , Mabibo, Mburahati ,Makurumla na Makuburi hawana sababu ya kwenda kulipia Manispaa ya Ubungo Makao Makuu.

pia Halimashauri imekuwa ikiangalia namna ya kuboresha masoko yote yaliyoko katika Manispaa ya Ubungo ikiwemo kuyasimamia mfano Soko la Ndizi Mabibo. lakini pia kubaini Maeneneo ya Uwekezaji kwa lengo la Kuongeza Mapato.

**Sekta ya Kilimo na Mifugo.**

Katika kilimo Manispaa ya Ubungo imeweza kuhimiza wananchi na wakazi wake kijikita katika kilimo cha mjini ( Protected Agriculture ) kilimo ambacho hutumia sehemu ndogo ya ardhi lakini huleta tija kwa jitihada hizo zimejidhihirisha wakati wa maonyesho ya Nanenane Mkoani Morogoro mwaka 2017 ambapo Manispaa ya Ubungo iliibuka kidedea kwa kutoa Mkulima bora ngazi ya Wilaya na Mkoa ndugu Fransis ambaye ni Mkulima wa nyanya katika kata ya Mbezi Manispaa ya Ubungo.

Kwa upande wa Mifungo Manispaa imejiwekea utaratibu wa kuwatembelea wafugaji na kuwapa elimu juu ya Ufugaji bora lakini pia Manispaa imeenda mbali zaidi kwa kuanzisha network za wafugaji ambazo huwawezesha kubadilishana maarifa juu ya mbinu bora za ufugaji na kuongeza Masoko ya bidhaa zao.

**Utawala na Uumishi.**

Utawala na utumishi ndiyo ingini ya Manispaa kwa kipindi cha mwaka mmoja Manispaa imeweze kusimamia watumishi ikiwa kuhakisha wale wote waliokuwa na vyeti feki kwa mjibu wa maagizo ya Serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Rais John P. Magufuli wanaondolewa katika utumishi wa Umma pia kuendelea na mchakato wa kuajili watumishi ikiwemo kada ya wasaidizi wa wahasibu katika kata na watendaji wa Mitaa pia Madereva.

kiujumla Manispaa imekuwa ikihakikisha watumishi wote wanafanya kazi zao kwa mjibu wa kanuni na taratibu za kiutumishi na wanapatiwa sitahiki zao.

**Mwisho** Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo kwa kipindi cha mwaka mzima imekuwa ikifanya viziuri katika maeneo mengine ya Miundo mbinu, Elimu Ardhi na Mipango Miji pia katika kuhabarisha Umma juu ya shughuli anuai ambazo zinatekelezwa na Manispaa ya Ubungo kwa wananchi wake.



*Moja ya mkakati wa kuongeza mapato ya halmashauri kwa kuongeza vitendea kazi ,magari 5 yaToyota hilux yalinunuliwa kwa ajili ya kutumika kukusanya mapato katika kata.*